JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KAZI NA AJIRA

MPANGO WA UTEKELEZAJI (PLAN OF ACTION) WA AZIMIO LA WAKUU WA MIKOA KUHUSU KUKABILIANA NA TATIZO LA UKOSEFU WA AJIRA KWA VIJANA, TANZANIA BARA

Dodoma,Tanzania

20 Novemba 2014

MWONGOZO WA UTEKELEZAJI (PLAN OF ACTION) WA AZIMIO LA WAKUU WA MIKOA KUHUSU KUKABILIANA NA TATIZO LA UKOSEFU WA AJIRA KWA VIJANA, TANZANIA BARA

1. Utangulizi

Mwongozo wa Utekelezaji unaelezea kwa kina makubaliano yaliyofikiwa katika Azimio la Wakuu wa Mikoa kuhusu namna ya kutatua tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana. Kupitia Mwongozo huu, Mikoa inaelekezwa namna ya kuandaa na kutekeleza mipango yao ya muda mfupi, kati na mrefu ya kukuza fursa za ajira na kupunguza umaskini. Mwongozo huu unaweka utaratibu na malengo muhimu kwa mikoa kuandaa mipango ya utekelezaji kulingana hali na mahitaji halisi ya mkoa husika.

Ili kuhakikisha utekelezaji endelevu wa Azimio la Wakuu wa Mikoa kuhusu kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira, mwongozo huu umeweka malengo, vipaumbele na mikakati ya utekelezaji.

1.1 Lengo la Mwongozo wa utekelezaji

Lengo la mwongozo huu ni kubadilisha mwelekeo uliopo wa ukosefu wa ajira na ajira isiyotimilifu kwa vijana ili kupunguza umasikini na kuboresha hali ya maisha ya Watanzania.

Muongozo huu umeainisha maeneo ya vipaumbele muhimu vifuatavyo:

1.2 Maeneo ya Kipaumbele

1.2.1 Kuwajengea vijana uwezo katika stadi za kazi na ujasiriamali.

1.2.2 Kuwapatia vijana maeneo ya uzalishaji na biashara ili kuwahamasisha kushiriki katika shughuli za kiuchumi hususan kilimobiashara.

1.2.3 Kuwezesha upatikanaji wa mitaji, nyenzo na vifaa vya uzalishaji mali kwa vijana.

1.2.4 Kuweka mfumo/utaratibu wa kuhamasisha ukuzaji wa ajira, uwekezaji na matumizi sahihi ya nguvukazi.

1.2.5 Kuimarisha mifumo ya utoaji wa taarifa za soko la ajira.

2. MWONGOZO WA UTEKELEZAJI (PLAN OF ACTION)

Mwongozo wa Utekelezaji umejikita katika maeneo yaliyobainishwa kama vipaumbele katika kutekeleza Azimio la Wakuu wa Mikoa. Kila eneo la kipaumbele lina lengo, mikakati na hatua za kuchukua.

MAENEO YA KIPAUMBELE

2.1 Kuwajengea vijana uwezo katika stadi za kazi na ujasiriamali

Shughuli za kiuchumi katika sekta rasmi na zisizo rasmi zinahitaji watu wenye ujuzi wa kiufundi (technical skills), elimu ya ujasiriamali na stadi za maisha (lifeskills). Vijana wengi wamesoma shuleni na vyuoni na wamehitimu kwa sifa za hali ya juu lakini sifa hizo hazilingani na ujuzi unaotakiwa katika soko la ajira. Hivyo vijana hawa wanahitaji kujengewa uwezo ili waweze kujiajiri au kuajiriwa.

2.1.1 Lengo

Kuondoa au kupunguza tofauti zilizopo kati ya ujuzi walionao vijana na ule ambao unahitajika katika soko la ajira.

2.1.2 Mikakati/Hatua za kuchukua

- Kubaini vijana na mahitaji yao ya ujuzi waliopo katika ngazi ya wilaya;
- Kutoa mafunzo ya ujasiriamali na stadi za kazi kwa vijana wenye mahitaji;
- Kutoa huduma za kitaalamu katika maeneo ya uzalishaji mali ya vijana;
- Kuhamasisha vijana kushiriki katika shughuli za kiuchumi za kujiajiri;
- Kuelimisha watendaji wa ngazi mbalimbali juu ya wajibu wao katika kukuza ajira kwa vijana.

2.2 Kuwapatia vijana maeneo ya uzalishaji na biashara ili kuwahamasisha kushiriki katika shughuli za kiuchumi hususan kilimobiashara

Kuwepo kwa maeneo mahususi kwaajili ya uzalishaji na biashara ni suala la muhimu katika kukuza ajira kwa vijana. Tatizo la ukosefu wa maeneo ya uzalishaji na biashara limesababisha vitendo vya uvunjifu wa amani katika maeneo mbalimbali nchini kutokana na vijana kuvamia maeneo yasiyo rasmi na kufanya shughuli za kiuchumi na kujiajiri. Mamlaka husika zimekua zikiwaondoa vijana hawa katika maeneo wanayofanyia shughuli zao na hatimaye kusababisha vurugu. Hivyo kutokuwepo kwa maeneo

maalum yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji na uzalishaji ni tatizo kwa vijana wahitimu ambao kwa hali ya sasa wakitaka kujishughulisha na kilimo ni lazima wawe na pesa za kununua mashamba. Hali hii imesababisha vijana wengi ambao wapo tayari kufanya shughuli za kilimo na ufugaji kukata tamaa. Hivyo, ni vyema ukawepo utaratibu wa kutenga maeneo maalumu ya uzalishaji na biashara kwa vijana kama inavyofanyika kwa upande wa wawekezaji wakubwa kupitia Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi (EPZA).

2.2.1 Lengo

Kuondoa vikwazo vinavyokwamisha vijana kupata maeneo ya kujishughulisha katika shughuli za kiuchumi hususan kilimo, biashara na uzalishaji.

2.2.2 Mikakati/Hatua za kuchukua

- Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga maeneo mahsusi ya vijana ya uzalishaji na biashara;
- Kuainisha maeneo maalum ya makazi na uzalishaji kwa ajili ya vijana (Youth Special Economic Zones);
- Kuwezesha vijana kufikiwa na huduma za kuendeleza biashara na kilimo ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa wataalamu wa kilimo na mifugo;
- Kuhakikisha upatikanaji wa miundombinu muhimu kama vile umeme, barabara, mawasiliano na huduma za kijamii katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uzalishaji na biashara.

2.3 Kuwezesha upatikanaji wa mitaji, nyenzo na vifaa vya uzalishaji mali kwa vijana

Tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana limechangiwa sana na ukosefu wa fursa za mitaji ya fedha, vifaa na nyenzo za kufanyia kazi. Ukosefu huu wa fursa za mitaji umetokana na kuwepo kwa masharti magumu ya kupata mikopo. Masharti haya ni pamoja na kuwa na mali zisizohamishika, hali ambayo imesababisha vijana wengi kushindwa kuanzisha shughuli za uzalishaji na hatimaye kujiajiri na kuajiri wengine.

2.3.1 Lengo

Kuanzisha huduma za kutosha na rahisi za mikopo kwa vijana ili kuongeza uwezo wa vijana hatimaye wajiajiri na kuajiri.

2.3.2 Mikakati/Hatua za kuchukua

- Kutenga rasilimali fedha kwa ajili ya kuwezesha shughuli za kuendeleza vijana;
- Kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana walio tayari kuanzisha shughuli za kiuchumi;
- Kuhamasisha jamii kuwa nautamaduni wa kuweka akiba na kuunda mifumo ya mikopo midogo kama vile SACCOS, Benki za Jamii na Asasi nyingine za mikopo.

2.4 Kuweka mfumo/utaratibu wa kuhamasisha ukuzaji wa ajira, uwekezaji na matumizi sahihi ya nguvukazi

Kukosa ushirikiano na uratibu sahihi miongoni mwa wadau, hasa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi na Vyama vya Kiraia wakati wa kushughulikia masuala ya ajira husababisha kukosekana mwafaka katika utekelezaji, na wakati mwingine huleta tatizo badala ya kulipunguza. Uwepo wa uratibu wa masuala ya ajira kuanzia ngazi ya wilaya kutaziba pengo kati ya watunga sera na utekelezaji wa sera na mipango.

2.4.1 Lengo

Kuwa na miundo na mifumo ya kurahisisha utekelezaji wa program mbalimbali za kukuza ajira kwa vijana.

2.4.2 Mikakati/Hatua za kuchukua

- Kuanzisha na kuendeleza dawati la uratibu wa masuala ya ajira katika ngazi ya Mkoa na Wilaya;

- Kuhakikisha kuwa suala la ukuzaji wa ajira linakuwa agenda ya kipaumbele na ya kudumu katika vikao vya Kamati za Ushauri za Mikoa (RCCs) pamoja na Mabaraza ya Madiwani na kamati zake katika Wilaya;
- Kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kwa kuwapatia mahitaji/huduma muhimu ili waweze kuanzisha miradi itakayowezesha kuongeza ajira katika ngazi ya wilaya;
- Kuhamasisha matumizi ya nguvu kazi iliyopo katika eneo husika katika utekelezaji wa miradi ya kijamii (public works) katika sekta

mbalimbali ikiwemo ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara, shule, vituo vya afya, n,k;

- Kuhakikisha kuwa suala la ukuzaji wa ajira kwa vijana ni agenda ya kuzingatiwa katika kutoa zabuni za miradi ya serikali katika ngazi za mkoa na wilaya;
- Kuhakikisha kuwa Mikoa, Wilaya na Halmashauri zinabainisha na kutangaza kwa umma huduma na bidhaa zinazozalishwa na vikundi vya wajasiriamali wanaopatikana katika maeneo husika na kuhimiza matumizi ya bidhaa na huduma za ndani katika ofisi za umma mfano, samani za ofisi n,k kwa ajili ya kuchochea uzalishaji na ajira.

2.5 Kuimarisha mifumo ya utoaji wa taarifa za soko la ajira

Taarifa za soko la ajira ni miongoni mwa vigezo vinavyotoa taswira halisi ya mafanikio ya kiuchumi na kimaendeleo kwa nchi au mahali husika. Taarifa za soko la ajira zina umuhimu wa kipekee katika kupanga, kutekeleza na kupima ufanisi wa mipango ya kiuchumi pamoja na kupima uwezo wa kiuchumi katika wakati husika.

2.5.1 Lengo

Kuweka mfumo wa kutoa taarifa za soko la ajira ambao unatoa taarifa za kutosha na kuwezesha michakato ya mipango na utoaji wa maamuzi katika ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa.

2.5.2 Mikakati/Hatua za kuchukua

- Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya masuala ya ajira kuweka utaratibu maalumuwa kukusanya takwimu za ajira;
- Kuandaa taarifa ya hali ya ajira ya Wilaya/Mkoa na kuwasilisha kwa Wizara yenye dhamana ya masuala ya ajira.

3 HITIMISHO

Ili kufikia mafanikio yaliyokusudiwa katika Mwongozo wa Utekelezaji wa Azimio la Wakuu wa Mikoa kunahitajika ushirikiano na ushirikishwaji wa wadau wote wa sekta binafsi na umma kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa. Hivyo utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa katika mwongozo huu utaweza kuzalisha ajira iwapo kutakuwa na mazingira bora ya ushirikishwaji wadau, juhudi katika upatikanaji wa rasilimali na utashi wa kisiasa.